

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anuani ya simu "ELIMU"  
Simu: 026 296 35 33  
Baruapepe: [info@moe.go.tz](mailto:info@moe.go.tz)  
Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)

**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb. Na. ED/OKE/NE/W/VOL.I/I/103**



Chuo cha Masomo ya Biashara  
na Sheria,  
Chuo Kikuu cha Dodoma  
(UDOM), Jengo Na. 10,  
S.L.P. 10,  
**40479 DODOMA.**

**Tarehe: 10 Desemba, 2018.**

Katibu Mkuu,  
Ofisi ya Rais TAMISEMI,  
S.L.P. 1923,  
**DODOMA.**

Mwenyekiti,  
TAMONGSCO,  
S.L.P. 63088,  
**DODOMA.**

Katibu Mtendaji,  
Christian Social Service Commission (CSSC),  
S.L.P. 1454,  
**DAR ES SALAAM.**

Katibu Mtendaji,  
Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA),  
S.L.P. 21422,  
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,  
Tanzania Association of Private Investors in Education (TAPIE),  
S.L.P. 13346,  
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,  
Baraza la Sunnah Tanzania, (BASUTA),  
S.L.P. 8581,  
**DAR ES SALAAM.**

## **WARAKA WA ELIMU NA. 2 WA MWAKA 2018**

### **UTARATIBU WA KUKARIRI DARASA KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI**

Serikali imekuwa na utaratibu wa kupokea na kushughulikia maombi ya kukariri darasa kutoka kwa baadhi ya wazazi na walezi wa watoto wanaoshindwa kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali. Aidha, Shule Zisizo za Serikali zimekuwa zikiwakaririsha darasa wanafunzi wanaoshindwa kufikia viwango vya ufaulu vinavyopangwa na shule husika.

Kufuatia hali hiyo kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wazazi na walezi kutokana na kutoshirikishwa ipasavyo katika kufanya uamuzi wa mwanafunzi kukariri darasa. Kutokana na changamoto zinazojitokeza kwenye suala hili wizara inapenda kutoa maelekezo kama ifuatavyo:

#### **1.0 Kukariri Darasa**

Maombi ya Kukariri darasa kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari yatashughulikiwa kama ifuatavyo:

- (a) Maombi ya Kukariri darasa la **I, II na III** yatashughulikiwa na Halmashauri husika ambapo darasa la **IV, V na VI** kwa Shule za Msingi na kidato cha **1, 2, 3, na 5** kwa shule za Sekondari yatashughulikiwa na Mkoa;
  - (b) Maombi ya kukariri darasa la **VII** kwa shule za Msingi na Kidato cha **4 na 6** ambayo ni madarasa ya mitihani ya mwisho ya Kitaifa yataendelea kutumwa kwa Kamishna wa Elimu ili kupata kibali cha kukariri; na
  - (c) Mwanafunzi atakayeomba na kukubaliwa kukariri katika ngazi ya Elimu ya Msingi na Sekondari atapewa fursa ya kukariri mara moja. Endapo mamlaka inayohusika itaona umuhimu wa Mwanafunzi kukariri darasa mara ya pili, atawezza kupewa fursa hiyo.
- (d) **Utaratibu wa Maombi ya Kukariri Darasa**
    - i. Mzazi wa mwanafunzi wa darasa la **I, II na III** anatakiwa kuandika barua ya maombi ya kukariri darasa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika;
    - ii. Mzazi wa mwanafunzi wa darasa la **IV, V na VI** kwa shule za Msingi na Kidato cha **1, 2, 3, na 5** kwa shule za Sekondari anatakiwa kuandika barua kwa Katibu Tawala wa Mkoa;

- iii. Mzazi wa mwanafunzi wa darasa la VII kwa Shule za Msingi na Kidato cha 4 na 6 kwa shule za Sekondari anatakiwa kuandika barua kwa **Kamishna wa Elimu** kulingana na darasa husika;
- iv. Maombi yote yapitie kwa Mkuu wa Shule anayosoma mwanafunzi na Mkurugenzi wa Halmashauri husika, na
- v. Kila barua ya maombi ni lazima iwe na viambatisho vifuatavyo:
  - a. Picha 2 za mwanafunzi aina ya pasipoti;
  - b. Namba ya kuandikishwa shulenii; na
  - c. Nyaraka zozote muhimu kulingana na sababu ya maombi yanayowasilishwa.

## **2.0 Kukariri Darasa Wanafunzi Wanaoshindwa Kufikia Viwango vya Ufaulu Vilivyowekwa na Shule**

Wizara inakumbusha kuwa wanafunzi waliofaulu mitihani ya upimaji inayofanywa kitaifa (Darasa la IV na Kidato cha 2) wanakuwa na sifa ya kumaliza ngazi ya elimu husika bila kukariri.

Hata hivyo, kwa makubaliano ya maandishi kati ya mzazi au mlezi na Mkuu wa shule ya Serikali au isiyo ya Serikali, mwanafunzi ataruhusiwa kukariri Darasa kwa kufuata utaratibu ulioainishwa hapo juu ambapo mzazi atakuwa ameridhia.

Waraka huu unafuta nyaraka zote zilizotangulia zilizokwu zikitoa maelekezo kuhusu utaratibu wa kukariri darasa na utanza kutumika **Januari, 2019**.



Dkt. Edicome C. Shirima  
**KAIMU KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:** Makatibu Tawala wa Mikoa,  
Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji,  
Wathibiti Ubora wa Shule Wakuu Kanda na Wilaya.

